



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Thelathini na Mbili – Tarehe 10 Juni, 2022

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

MASWALI:

Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

145. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Serikali imekuwa ikijitahidi kueneza na kuboresha huduma ya maji mijini na vijijini Unguja na Pemba. Hata hivyo, katika kijiji cha Kilimni ndani ya jimbo la Pandani kumekuwa na ukosefu wa maji salama ya mfereji (bomba) kwa takriban miaka 19 na yaliyopo hayana huduma ya kutiwa dawa. Aidha, mashine ya kusukumia maji (pump) kubwa iliyokuweko ilipelekwa sehemu nyengine na badala yake kuletwa ndogo ambayo haina uwezo wa kutosha.

- (a) Je, ni lini Serikali itawapatia wananchi wa Kilimni mashine yao kubwa ya kusukuma maji.
- (b) Je, ni lini Serikali itaanza kuyapatia huduma ya dawa maji yapatikanayo katika kijiji cha Kilimni.
- (c) Je, ni upi mpango wa Serikali wa kuwapatia wananchi wa Kilimni maji ya kutosha na salama ya mfereji na yenye dawa.

Wizara ya Afya:

114. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa Zanzibar pamoja na nchi nyengine za Afrika Mashariki na zile zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara kumekuwa na ongezeko kubwa la maradhi yasiyo ya kuambukiza (Non Communicable diseases) kama vile kisukari (Diabetes mellitus) pamoja na "pressure" ya kupanda na kushuka yaani (hypo and hypertension) maradhi ambayo yamekuwa yakipoteza rasilimali watu siku hadi siku. Na kwa kuwa wazanzibari hawana tabia ya kuchunguza afya zao hadi pale wanapoumwa jambo ambalo linasababisha tatizo hilo kuwa kubwa zaidi.

Je, ni lini Serikali yetu itaandaa utaratibu maalum wa kuitisha timu ya maafisa wa afya kwenye miji, vijiji na vitongoji kwa ajili ya kuwachunguza wananchi magojwa haya.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

99. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Viongozi mbali mbali wa Serikali waliahadi kujengwa kwa barabara ya Wawi kwa Dkt. Omar Ali Juma, barabara ambayo inaunganisha barabara kuu ya Uwanja wa Ndege. Katika kumuenzi kiongozi huyo pamoja na kutimiza ahadi za muda mrefu zilizotolewa.

Je, ni lini barabara hiyo itajengwa

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

151. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Ni mazao gani ya chakula na biashara yanauzika nje ya nchi ukitoa zao la karafuu hapa kwetu Zanzibar.

Zanzibar,
10 Juni, 2022.



(Raya Issa Msellel)
KATIBU WA BARAZA